# MSWADA: Sababu 50 za kuunga mkono, dhidi ya sababu 15 za kuupinga Mswada wa sheria ya vyama vya Siasa Tanzania, wa Oktoba 2018.

## A. SABABU 50 ZA KUUNGA MKONO.

1. Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itakuwa na jukumu la kusajili vyama vya siasa.

2. Kutoa elimu ya uraia ni jukumu la pili la Ofisi ya msajili wa vyama vya siasa,

3. Ofisi ya Msajili kuwa ndiye msimamizi wa mienendo ya vyama vya siasa vyote nchini Tanzania.

4. Mswada unapendekeza kwamba Ofisi ya msajili wa vyama vya siasa itasimamia utekelezaji wa Sheria katika vyama vya siasa.

5. Mswada huu utasaidia Kurekebishwa kwa kuondoa matumizi ya maneno ~~“wasajili wasaidizi”~~ na badala yake kutumia neno “wakurugenzi”.

6. Mswada huu utasaidia taasisi zenye nia ya kutoa elimu ya uraia nchini kumtaarifu Msajili.

7. Mswada huu unapendekeza kumwezesha Msajili kupata taarifa kutoka katika chama chochote cha siasa.

8. Unapendekeza kumuwezesha Msajili kuratibu utoaji wa elimu ya uraia.

9. Kifungu cha 6A kinachopendekezwa kitawezesha vyama vya siasa kufuata matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Katiba ya Zanzibar na Sheria ya Vyama vya Siasa.

10. Mtu anayeweza kuomba kusajili chama cha siasa kwamba anapaswa kuwa ni raia wa Tanzania mwenye umri zaidi ya miaka 21 na wazazi wake wote wawili wawe ni raia wa Tanzania.

11. Kifungu cha 6C kinaweka vigezo vya mtu kuwa mwanachama wa chama cha siasa na pia kuzuia mtu asiye raia kushiriki katika shughuli za chama cha siasa Tanzania.

12. Mwanachama wa chama cha siasa ni lazima awe ni Raia wa Tanzania.

13. Mtu anapaswa kuwa ni mwanachama wa chama kimoja tu.

14. Mtu atakapo jiunga na chama kingine cha siasa ni lazima arudishe kadi ya chama cha kwanza.

15. Mwanachama anaweza kufukuzwa tu kutoka katika chama chake kwa kufuata taratibu za Katiba ya chama husika cha siasa.

16. Kifungu cha 8 kinapendekezwa kurekebishwa ili kuweka masharti ya ukomo wa usajili wa muda kwa vyama vya siasa vilivyoomba usajili kamili na vile ambavyo havijaomba usajili kamili.

17. Chama cha siasa kitakamilisha usajili wake wa kudumu baada ya kupewa cheti cha usajili wa kudumu.

18. Chama hakitasajiliwa ikiwa jina, ufupisho wa jina au alama, rangi na nembo ya chama inafanana na ya chama kingine.

19. Chama hakitatumia alama au rangi ya chama ambacho kimefutwa au usajili wake umekwisha muda wake.

20. Kifungu cha 8A Msajili kutunza rejesta za vyama vya Siasa. kinataja rejesta ambazo zitatunzwa na Msajli kwamba ni:-

21. Rejesta hizi zitajumuisha rejesta ya vyama vya siasa.

22. Rejesta ya viongozi wa kitaifa wa vyama na

23. Rejesta ya wajumbe wa bodi ya wadhamini ya chama cha siasa.

24. Kuweka katazo kwa vyama vya siasa kuanzisha vikundi vya ulinzi na usalama,

25. Katazo la kuendesha mafunzo ya kutumia nguvu au silaha vya aina yoyote kwa wanachama wake.

26. Unapinga chama cha siasa kuendesha shughuli za Kiharakati.

27. Kuhakikisha kuwa uanachama katika vyama vya siasa uko wazi kwa watu wenye ulemavu.

28. Kuhakikisha chama chochote khakiruhusu mmomonyoko wa umoja wa kitaifa na kutumia dini kutimiza malengo yake.

29. Kuvitaka vyama vya siasa kuwa na wanachama wasiopungua mia mbili wenye vigezo vya kusajiliwa kama wapiga kura kutoka mikoa ya Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

30. Kumpa Msajili mamlaka ya kuhakiki vyama wakati wowote ili kuhakikisha utekelezaji na uzingatiaji wa masharti ya usajili.

31. Kuongeza vigezo anavyopaswa kuwa navyo mtu anayegombea nafasi ya uongozi wa chama cha siasa.

32. Mswaada huu utajumuisha uchaguzi wa Baraza la Wawakilishi na wabunge wa Baraza la Wawakilishi.

33. Kuweka masharti yahusuyo kuungana kwa vyama vya siasa.

34. Kuweka ukomo wa vyama vilivyoungana na ushirika wa kisiasa baina ya vyama vya siasa.

35. Uamuzi wa kuunganisha vyama utafanywa katika mkutano mkuu wa chama.

36. Vyama vilivyoungana vitafutiwa usajili na kitasajiliwa chama kipya kilichoundwa.

37. Kifungu cha 12A kuvitaka vyama vya siasa kuwasilishwa kwa Msajili tamko la mapato yote na matumizi.

38. Kifungu cha 13 chanzo chochote cha mapato kinachopatikana nchini vinavyopaswa kuwekwa wazi kwa Msajil.

39. Chama cha siasa baada ya kusajiliwa kinapaswa kueleza mali zake, rasilimali vitu, viwanja mashamba ofosi, shule, hosipitali n.k.

40. Kuvitaka vyama vya sisasa kuteua afisa masuhuli atakaesimamia mali za chama.

41. Kuvitaka vyama vya siasa kuwa na akaunti ya benki tofauti kwa ajili ya fedha za ruzuku.

42. Kumuwezesha Msajili kusitisha ruzuku kwa chama cha siasa pale ambapo anaamini kuwa chama husika kimeshindwa kusimamia fedha hizo.

43. Msajili kumuomba Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum katika matumizi ya Ruzuku ya Chama.

44. Kuvitaka vyama vya siasa kuwasilisha taarifa za hesabu zao kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi.

45. Chama kuwasilisha taarifa ya hesabu zilizokaguliwa kwa Msajili.

46. Kumwezesha Msajili kufuta usajili wa chama cha siasa kitakachobainika kuwa kilipata usajili kwa njia zisizo halali.

47. Kumuwezesha Msajili kusitisha usajili wa chama cha siasa kitakachovunja masharti ya Sheria.

48. Kuzuia viongozi wa vyama vya siasa kutokuwa wajumbe wa bodi ya wadhamini.

49. Mswada huu utaliwezesha Baraza la Vyama vya Siasa kupata fedha kutoka katika bajeti ya Serikali na wafadhili.

50. Mwisho, kifungu cha 22 kinapendekezwa kufanyiwa marekebisho ili kumpa Waziri mamlaka ya kutengeneza kanuni za uandaaji wa taarifa za hesabu za vyama vya siasa na mambo yatakayojumuishwa katika Katiba za vyama.

**B. SABABU 15 ZA KUUPINGA MSWADA WA VYAMA VYA SIASA.**

1. Unakiuka Katiba ya nchi na unaokataza uhuru wa kujumuika.

2. Vyama vya upinzani havikushirikishwa katika kuandaa mswada wa vyama vya siasa hata pale ulipotoa maoni hayakutokea kabisa katika mswada huu

3. Shughuli za vyama vya siasa sasa kuwa kosa la jinai.

4. Msajili wa vyama vya siasa amejipa mamalaka makuwa na kuweza kuingilia shughuli za siasa, anapaswa kuwa mlezi wa vyama na sio kuwa mwamuzi wa musho.

5. Kabla hata sheria kutungwa msajili tayari amesha tunga kanuni na kuziwasilisha katika baraza la vyama.

6. Mswada umeleta marekebisho mengi ambayo yanauwa msingi wa kutungwa kwa sheria ya vyama vya siasa namba 5 ya mwaka 1992.

7.Mswada umejaa adhabu za jinai na kufanya shughuli za kisiasa kuwa jinai.

8. Msajili wa vyama vya siasa kuingilia chaguzi za ndani ya vyama.

9. Mafunzo ya kiraia yatolewe na asasi za kitanzani na sio za nje, wan je akitaka kutoa elimu aombe kibali kwa msajili lengo ni kuinyima jamii elimu ya uraia.

10. Msajili kulazimisha Vyama kuwa na katiba zinazofanana.

11. Unazuia Chama kuwa ulinzi.

12. Waziri atatunga kanuni za vyama kuungana ataua upinzani.

13. Unampa masajili mamlaka ya kumsimamisha na kumfukuza mwanachama.

14. Unapinga chama cha siasa kuendesha shughuli za Kiharakati ambalo ndilo jukumu la upinzani.

15. Msajili wa vyama vya siasa kupewa kinga ya kutokushitakiwa anapotekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii.

MWISHO.